



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

LIBRARY FB ATTORNEYS

UZINGATIAJI WA MASHARTI YA USAJILI YA TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Dodoma, Tanzania – Januari 10, 2025

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) inapenda kuwakumbusha taasisi zote za umma na binafsi kwamba muda wa usajili wa hiari, kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ulimalizika tarehe 31 Desemba, 2024. Agizo hili, lililotolewa wakati wa uzinduzi wa PDPC, lilionesha dhamira ya Serikali kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya mwaka 2022.

PDPC inatambua juhudi za taasisi ambazo tayari zimesajiliwa. Pamoja na jitihada hizo, Tume imebaini idadi kubwa ya taasisi ambazo hazijaanza kabisa zoezi la kujisajili ukiacha taasisi chache ambazo bado hazijakamilisha usajili. Ikumbukwe kwamba, Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ilianza kufanya kazi tangu tarehe 01 Mei, 2023, hivyo basi kutokuzingatia matakwa ya Sheria hiyo, kunahatarisha juhudi za Serikali za kulinda haki za faragha na taarifa binafsi za wananchi na pia kunadhoofisha uadilifu katika kuboresha usimamizi wa maendeleo ya uchumi wa kidijitali nchini.

Ili kutoa fursa ya mwisho kwa taasisi ambazo hazijajisajili kabisa na ambazo hazijakamilisha usajili hadi sasa, PDPC inaongeza muda wa mwisho wa usajili hadi kufikia tarehe **30 Aprili, 2025**. Taasisi zitakazoshindwa kujisajili ndani ya muda huu zitachukuliwa hatua kali za kisheria, zikiwemo adhabu na hatua nyingine zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

USAJILI WA LAZIMA

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 na 21 cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, taasisi zote za umma na binafsi zinazokusanya, kuchakata, au kuhifadhi taarifa binafsi zinatakiwa kusajiliwa na PDPC kupitia Mfumo wa Usajili na Uzingatiaji (RCMIS) unaopatikana kwenye tovuti rasmi ya PDPC: www.pdpc.go.tz.

UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA (COMPLIANCE AND ENFORCEMENT) KUANZA TAREHE 1 MEI, 2025

Kuanzia tarehe **1 Mei, 2025**, PDPC kwa kushirikiana na vyombo vya utekelezaji wa sheria, itaanza kuchukua hatua za kisheria dhidi ya taasisi zote ambazo hazijazingatia matakwa ya Sheria husika. Taasisi ambazo zitabainika hazijasajiliwa zitakabiliwa na adhabu za kisheria,

Makulu Street, 10 UCSAF Road, P.O Box 1105, 41107 DODOMA, Phone: +255 743 699 996
email: dg@pdpc.go.tz, Website: www.pdpc.go.tz

“Faragha Yako Ni Wajibu Wetu”

ikiwemo faini kubwa na hatua nyingine za utekelezaji kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

PDPC itaendelea kutoa elimu, maelezo na miongozo kwa umma na kwa taasisi zinazofanya mchakato wa usajili. Aidha, jitihada za kuongeza uelewa wa umma kuhusu dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi na mahitaji ya uzingatiaji zitaimarishwa katika kipindi hiki.

WITO

PDPC inasisitiza kwamba kulinda taarifa binafsi ni jukumu la kisheria na msingi wa ajenda ya mabadiliko ya kidijitali nchini. Uzingatiaji si tu hitaji la kisheria bali pia ni kiashiria cha uwajibikaji wa taasisi na dhamira ya kulinda haki za wananchi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 16(1).

Tunatoa wito kwa taasisi zote ambazo bado hazijasajiliwa kuchukua fursa hii ya mwisho na kutimiza wajibu wao wa kisheria. Kutokuzingatia Sheria hakutavumiliwa baada ya muda wa nyongeza wa usajili kukamilika.

Kwa maelezo zaidi au msaada, tafadhali wasiliana na PDPC kupitia:

- **Barua pepe:** helpdesk@pdpc.go.tz
- **Nambari za Simu:** +255 718462536 / 0744057652 / 0753459155 / 0695507751 / 0615779070
- **Tovuti:** www.pdpc.go.tz

Tushirikiane kujenga mustakabali wa ulinzi wa taarifa unaojengwa juu ya imani, uwajibikaji, na usimamizi salama wa taarifa na faragha binafsi katika uchumi wa kidijitali unaokua wa Tanzania.

Imetolewa na:

Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia

Mkurugenzi Mkuu

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)